

Je, Umeingwa na Medicaid?



Unachohitaji kujua kuhusu kufanya upya huduma yako ya afya.

Kila mwaka, Jimbo hukagua taarifa za wanachama wa Medicaid ili kuhakikisha kuwa bado wanastahiki. Ikiwa tuna maelezo ya kutosha, tutakutumia notisi (Notisi ya Uamuvi wa Faida) kukuambia kwamba tumefanya upya Medicaid yako.

Ikiwa tunahitaji maelezo zaidi, **tutakutumia notisi mbili:**

- 1 Notisi ya manjano ya kufanya upya Medicaid.
- 2 Notisi nyeupe inayoomba hati za ziada.

Notisi hizi mbili zitatumwa kwa barua za posta tofauti. Hakikisha unangoja zote mbili.

Mambo 3 unayoweza kufanya ili kuwa tayari na kuendelea kukingwa.

1. **Sasisha maelezo ya akaunti yako** ili Jimbo liweze kukufikia kwa taarifa muhimu. Kwa mfano, unapaswa kusasisha akaunti yako ikiwa maelezo yako ya mawasiliano yamebadilika, umepata kazi mpya, au umepata mtoto.
2. **Ngoja barua kutoka Jimbo la Rhode Island.** Ikiwa mpango wa Medicaid utahitaji habari zaidi ili fanya upya huduma yako, utapata notisi ya njano. Pia utapata notisi nyeupe inayouliza hati za ziada. Vinginevyo, utapata notisi inayosema kwamba huduma yako imeendelea kiotomatiki.
3. **Chukua hatua mara moja.** Ukipata notisi ya njano, inamaanisha kuwa Serikali inahitaji maelezo zaidi kukuhusu wewe au watu wa kaya yako ili kufanya upya huduma yako. Tafadhalu wasilisha taarifa zote zilizoombwa kabla ya tarehe ya mwisho ya notisi yako.

Una Maswali?

Usaidizi unapatikana. Piga Simu:

- HealthSource RI 1.855.840.4774
- RI Idara ya Huduma za Binadamu 1.855.697.4347

Au dhibiti akaunti yako mtandaoni:

- HealthyRhode.RI.gov
- Programu ya simu ya HealthyRhode



Jifunze zaidi.

Ili kupata maelezo zaidi kuhusu kufanya upya Medicaid au uangalie wakati kufanya upya kutafanyika, tembelea staycovered.ri.gov au changanua msimbo wa QR.



Changanua msimbo wa QR
ili kuangalia tarehe yako ya kufanya upya Medicaid.



HealthSourceRI
WE WORK FOR YOU



KUWA TAYARI.
KAA UMEKINGWA.